**Noa Bongo – Jenga Maisha Yako ! – Utandawazi : Biashara Taasisi Ndogo za Mikopo Cameroon**

---

**O- Töne : Bernard Manyo**
**Autor : Sandrina Blanchard**
**Redaktion : Yann Duran**
**Übersetzung : Anne Thomas**

---

- **Junger sprecher 1 ………..Msimulizi wa kiume 1**
- **Junge sprecherin 1 ……….Msimulizi wa kike 1**
- **Sprecher(in) ………..Msimulizi wa kike 2**
  **al Off –Stimme für die Reportage**

**Für die O-Töne dazu :1 Mann, 1 Frau: Mwanaume 1Mwanamke1**

---

**Vorspann LbE …….Kiashirio cha Kipindi**

**SEHEMU YA 1 – REPORTAGE : REPOTI**

**Msimulizi wa kike 1 :** Habari gani !(Sprecher)

**Msimulizi wa kiume 1 :** Natumai nyote hamjambo! Leo katika mfululizo wetu kuhusu utandawazi tutazungumzia juu ya harakati za kuanzisha biashara.

**Msimulizi wa kike 1 :** Na tutakuwa tunaelekea Douala mji mkuu wa kibiashara nchini Cameroon.

**Msimulizi wa kiume 1 :** …….ambapo hapo tutakutana na mhandisi aliyebobea katika taaluma ya Teknolojia ya Habari IT na Mawasiliano ya Simu.

**1.Unternehmer Atmo 1 Tür (unterlegen)**

Tamanjong Sangjong anaanza harakati zake za kutwa kabla ya saa mbili asubuhi.Mhandisi huyo wa Cameroon mwenye umri wa miaka 40 ni meneja wa kampuni kubwa ya huduma ya Teknolojia ya Habari IT ijulikanayo kwa jina la Soft Tech International.

**Atmo hoch ?**

**Msimulizi wa kike 2 :** Ofisi ya Tamanjong iko katika eneo la maduka mengi ya nguo mjini Douala.Chumba chenyewe cha ofisi kingeliweza kuonekana kama cha Kiafrika ingelikuwa hakina mapambo lakini taratibu za biashara zinazotumiwa na Tamanjong na wafanyakazi wake moja kwa moja zinatoka Marekani.Huenda ikawa imesadifu tu lakini ofisi ya meneja imetengenezwa kushabihiana na umbo la yai.

**2. Unternehmer Tamanjong Gründung (1= 0-57)**

Kampuni ya Soft Tech imeanzishwa hapa nchini Cameroon hapo mwaka 1992….kwetu hii ilikuwa ni hatua ya maendeleo ya asili. Kwani kampuni hiyo kwanza kabisa ilianzishwa na mimi mwenyewe nchini Marekani hapo mwaka 1987.Kwa vile nilikuwa natoka Cameroon nilikuwa na hamu ya kurudi Cameroon hapo mwaka 1992.

**Msimulizi wa kike 2 :** Kwa hiyo Tamanjong aliamuwa kuondoka Marekani ili kuanzisha kampuni yake katika nchi alikozaliwa.Baada ya miaka michache kampuni hiyo ya Soft Tech ikaanza kujulikana katika soko la Cameroon kutokana na usimamizi wake mzuri wa kutowa huduma za Teknolojia ya Habari IT za aina mbali mbali.

**3. Unternehmer Tamajong Markt (1.29)**

Tumeona kwamba kuingia kwa simu za mkono barani Afrika kumekuwa mojawapo ya teknolojia za mafanikio pamoja na kuongeza vidoido ambavyo vilikuwa maalum kwa soko hilo na vilikuwa haviko kwenye soko ambavyo baadhi yao vilitengenezwa kwa haraka na kampuni au kuagiziwa kutoka nje.Kwa hiyo tukaamuwa kuwa na kitengo chenye kushughulikia kazi hiyo. Hadi sasa tumekuwa tukishughulikia zaidi taasisi za kifedha katika fani za benki na bima kadhalika na taasisi ndogo ndogo za kiuchumi na mikopo.Katika fani

ya mawasiliano ya simu tumekuwa tukiongeza huduma ikiwa ni pamoja na watu wanaojifunza kazi za kitaaluma.Pia huwa tunatowa ushauri elekezi katika fani ya huduma za mawasiliano ya simu na fedha kadhalika marekebisho ya mashirika ya fedha.

**4.Unternehmer Atmo conference room -…………chumba cha mikutano………..**

**Msimulizi wa kike 2** : Wahandisi 25 wa Teknolojia ya Habari IT wanafanya kazi na Tamanjong.Hutowa huduma zao kugharamia wafanyakazi waliobobea kitaaluma kuwasaidia kusimamia shughuli na kumbukumbu za kibiashara.Wafanyakazi wa kampuni ya Soft Tech huajiriwa kwa kuzingatia sifa walizonazo kitaaluma.Na yule mwenye kufaa anakuwa mhandisi au mtaalamu wa komyuta.
Lakini mara nyengine kampuni ya Soft Tech inabidi iwaajiri wahitimu wa chuo cha Polytech ambacho ni chuo cha uhandisi huko Yaounde.

**5.Unternehmer Tamanjong Einstellung (2.28)…………..**

Lakini inaonekana kama vile haitoshi na kunakuwepo na ushindani mkubwa kwetu sisi katika suala la kuwaajiri wahandisi bora lakini kuna kampuni kubwa kabisa za simu mjini ambazo zinataka kutupiku katika kuwania baadhi ya wanafunzi wanaohitimu kutoka chuoni.Lakini mbali na suala la rasilmali ya kibinaadamu ambalo ni suala la kimsingi lililofanywa kuwa zito kutokana na ukosefu wa kumjengea mtu uwezo wa kitaaluma katika sekta hii, hupendelea kuwafunza wahandisi vijana ndani ya kampuni ambao wanakuja tu kuwa wazuri wenye faida baada ya mwaka mmoja au miwili hivi.

**Msimulizi wa kiume 1:** Ningelipenda kuwa mhandisi wa IT……

**Msimulizi wa kike 1(mocking……dhihaki) :** Ingelifaa kwanza ujifunze namna ya kuchapisha makala kwenye kifaa cha kuchapia maneno….

**5.Atmo Tastatur**

**4. Atmo conference room hoch ………..chumba cha mikutano**

**Msimulizi wa kike 2 :** Kampuni ya Soft Tech ina chumba cha mikutano chenye kuchukuwa wateja wanane ambacho kiko pembeni tu mwa chumba cha meneja.Jessy Ayamoh anaongoza taasisi ndogo ya mikopo.Kampuni yake pia inatumia teknolojia ya kampuni ya Soft Tech.

**6.Unternehmer Kundin (5.51) ……(mteja)**

Kutokana na kutumia maelekezo ya kompyuta ya kampuni hiyo yaani kipi cha madeni na kipi cha kukopwa bila ya shaka utakuta una taarifa yako ya fedha ilio tayari na inakuwa rahisi sana kwa udhibiti wa kodi.

**Msimulizi wa kike 2 :** Mafanikio ya Tamanjong katika ngazi ya kienyeji ya ndani ya nchi yamemfanya ajulikane pia nje ya Douala.Kampuni ya Soft Tech hivi sasa inatanuka kuingia katika nchi nyengine za Kiafrika.

**7.Unternehmer Tamanjong 4.30**

Barani Afrika shughuli za mapatano ya kibiashara kutoka nchi moja kwenda nyengine yanakuwa magumu kidogo kufanyika kwa kulinganishwa na mabara mengine. Safari zikiwa nyingi baina ya nchi Kiafrika mara nyingi zinakuwa zinasumbuwa na kwa hiyo wakati unapoendesha shughuli zako katika kwenye nchi nyengine kwa kweli zinakuwa za gharama kubwa sana na zoezi gumu kutekelezeka.Tuna utashi na soko la Ghana ukweli ni kwamba tuna hata wateja nchini Ghana,benki ya western world nchini Ghana inatumia bidhaa zetu nchini Nigeria pia tuna taasisi chache ndogo ndogo za kifedha ambazo zimekuwa zikitumia bidhaa zetu.

**Msimulizi wa kiume 1:**
Kwa hiyo Tamanjong ni mfanyabishara mwenye mipango mingi

**Msimulizi wa kike 1 :**

Ndio ni kweli kabisa.Mpango wake ni kutanuka kuingia kwenye nchi nyengine kadri inavyowezekana.Kuteka masoko mapya.

Kampuni ya Soft Tech daima imekuwa ikibuni vitu vipya.

**Msimulizi wa kiume 1 :** Una maanisha nini kubuni ?

**Msimulizi wa kike 1 :**
Kampuni ya Soft Tech siku zote inakuwa inakuja na mawazo mapya kutengeneza bidhaa kabla ya hata washindani wao kuzifikiria.Kubuni moja kwa moja kunamaanisha kutengeneza kitu fulani kipya.

**8.Unternehmer Tamanjong**
Kimsingi utashi wetu ni kutowa ufumbuzi wa Kiarika katika sekta ya ya huduma za fedha.Hususan tumekuja na bidhaa ambayo tuko njiani kuizinduwa ambayo inaitwa Payters…haya ni maelekezo ya malipo yaliobuniwa Afrika kwa kuzingatia mfumo wa matumizi ya kompyuta ya mtandao wa GSM. Kimsingi huwa ni simu ya mkono ikiagiza malipo kwa mtu binafsi au kwa kampuni kwa kutumia tu akaunti yako ya kawaida ya malipo kwa kupitia simu ya mkono.

**Msimulizi wa kiume 1 :** Ohhh ……hiyo haina usumbufu !

**Msimulizi wa kike 1 :**
Kwa kadri utakavyoweza kujuwa namna ya kudhibiti fedha zako….iwapo utatumia zaidi kuliko kile ulichonacho unaweza kwa urahisi kutumbukia kwenye madeni.

**Msimulizi wa kiume 1 :** Lakini kile unachotakiwa kufanya ni kuchukuwa mikopo ….

**Msimulizi wa kike 1 :**
……..ambayo iko siku inabidi ulipe tena na riba juu yake ..lakini tutayazungumzia hayo huko mbele……….

**Msimulizi wa kike 2 :**
Muulize Tamanjong ni nini ufunguo wa mafanikio yake na hili ndio jibu lake:

**9.Unternehmer Qualität : (3.00)**

Ubora wa bidhaa ….huenda zikawa chini kuliko kile kinachoagizwa kutoka nje lakini kimsingi takriban wateja wetu wote kwa kweli wameshangazwa sana sana kwamba tuna uwezo wa kuongeza vidoido ambavyo vinalingana na viwango vyote vile vinavyotegemewa mahala popote pale duniani ambapo unategemea kuwa na kiwango bora kabisa.

**MWISHO SEHEMU YA KWANZA**

**Musik hoch dann unterlegne und ausblenden**

**SEHEMU YA PILI ERKLÄSTÜCK**

**Msimulizi wa kiume 1 na Msimulizi wa kike 1 tu !**

**Msimulizi wa kiume :**
Ulikuwa ukimaanisha nini hapo awali juu ya mikopo ?

**Msimulizi wa kike :**
Nilikuwa tu nataka nikukumbushe kwamba wakati benki inapokupa mkopo sio tu kwa ajili ya kukufurahisha …unachukuwa mkopo na riba.

**Msimulizi wa kiume :**
Sikufahamu ……

**Msimulizi wa kike :**
Juu ya kwamba ni jambo lililo wazi ……..iwapo benki inakubali kukukopesha fedha ni kwa sababu inataka kupata fedha zaidi kwa ajili yake yenyewe. Inabidi ulipe sio tu fedha ulizokopa bali pia fedha kidogo zaidi hadi pale deni lako litakapomalizika.

**Msimulizi wa kiume :**
Kwa hiyo kwa kadri nitakavyokuwa nalipa pole pole mkopo wangu ndivyo nitakapoishia kulipa zaidi? Iwapo nitachukuwa

miaka 300 kuulipa mkopo huo huenda nikaishia kulipa mara kumi zaidi kuliko kile benki ilichonikopesha mara ya kwanza?

**Msimulizi wa kike :**
Hasa ! Lakini mara nyengine hauna haja ya kusubiri miaka 300 kulipa mara kumi zaidi ya kile ulichokikopa.Hiyo ndio riba. Kadri riba inavyozidi kuwa kubwa ndivyo kima cha fedha unazotakiwa kuzirudisha kinavyozidi kuwa kikubwa.

**Msimulizi wa kiume :**

Katika mikopo hiyo pia walizungumzia juu ya mikopo midogo..

**Msimulizi wa kike :**

Mikopo midogo ni sehemu ya fedha zinazotolewa na taasisi ndogo za fedha.

**Msimulizi wa kiume :**

Ina maana zinakuwa kidogo sana au sivyo ?

**Msimulizi wa kike :**

Kwa usahihi tunaweza kusema ni elfu moja.Baadhi ya taasisi hujishughulisha maalum katika kutowa mikopo midogo midogo.Kwa ujumla kima cha fedha kinakuwa kidogo na kwa ajili ya mradi maalum.Kwa mfano mafundi stadi huenda wakahataji fedha kuanzisha biashara ndogo lakini kwa vile mafundi wanakuwa sio matajiri mabenki makubwa huwa na hofu kuwakopesha kwa kuwatilia mashaka iwapo wataweza kuzirudisha fedha zao.

**Msimulizi wa kiume :**

Kwa hiyo benki hazikopeshi watu maskini ?

**Msimulizi wa kike :**

Hapana hawakopeshi. Lakini maskini badala yake wanaweza kupata mkopo mdogo kutoka taasisi ndogo za fedha.

**Msimulizi wa kiume :**

Hizo taasisi ndogo za fedha ni taasisi gani ?

**Msimulizi wa kike :**
Taasisi ndogo za fedha huwa zinafanya kazi kwa kuzingatia msingi wa mshikamano lakini pia shughuli zake hujumuisha uwekaji wa fedha za akiba kwenye akaunti na bima ndogo ndogo.

**Msimulizi wa kiume (sarcastic….dhihaka ) :**
Mshikamano? Ni ubunifu wa aina yake !

**Msimulizi wa kike :**
Watu wamekuwa wakisaidiana kwa muda mrefu lakini katika miaka ya 1970 mikopo midogo midogo ikaanza kufanya kazi duniani kote.Umoja wa Mataifa unafikiri kwamba hiyo ni zana muhimu katika kupiga vita umaskini.Hapo mwaka 2006 mwanauchumi wa Bangladesh Mohammed Yunus alitunukiwa Tuzo ya Amani ya Nobel kwa mchango wake katika taasisi ndogo ndogo za mikopo.

**Msimulizi wa kiume :**
Naam hicho ndicho nitakachokifanya wakati nitakapokuwa mkubwa!

**Msimulizi wa kike :**
Unaweza kujaribu lakini tuzo ya Nobel tayari imechukuliwa!

**Outro ……………………Funga Kipindi…….**

**Msimulizi wa kike 2 :**

Na hapo ndio tumefikia mwisho wa kipindi chetu cha Noa Bongo Jenga Maisha Yako !Asante kwa kusikiliza kipindi hiki kuhusu utandawazi juu ya biashara na taasisi ndogo za mikopo.Ni kipindi che Deutsche Welle kilichotayarishwa na Sandrine Blanchard na Bernard Manyo.Ili kujuwa zaidi au ukitaka tena kusikiliza kipindi hiki nenda katika tovuti yetu www.de-world.de/be
Usikose kujiunga nasi tena mara nyengine.
Kwaheri !